Jina ______________________________________________ Nambari ________________________________

Sahihi ya mtahiniwa ____________________

Tarehe _________________________________

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**
**AGOSTI 2021**
**MUDA: 1 ¾**

# MTIHANI WA GOLDEN ELITE

# JUZUU YA KWANZA

**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**
**Muda: 1 ¾**

**MAAGIZO**

(a) Andika insha mbili.

(b) Swali la kwanza ni la lazima.

(c) Kisha chagua insha moja nyingine kutoka hizo tatu zilizobakia.

(d) Kila insha isipungue maneno 400.

(e) Kila insha ina alama 20.

*Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa*

Kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706

***Geuza ukurasa***

1. **Insha ya lazima.**
   Andika barua kwa Waziri wa Kilimo kupitia kwa Katibu wa Kilimo huku ukipendekeza jinsi nchi ya Kenya inavyoweza kukabiliana na janga la njaa.

2. Dawa za kulevya na pombe haramu ni tatizo sugu nchini. Eleza chanzo na utatuzi wa janga hili.

3. Siku ya kufa nyani miti yote huteteza.

4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno: Baada ya kukabidhiwa cheti cha matokeo, Mandi alizirai papo hapo kisha akakata roho. Sote tulimlaumu daktari kwa kumwambia ukweli.

Jina ______________________________________________ Nambari ________________________________

Sahihi ya mtahiniwa ____________________

Tarehe _________________________________

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**LUGHA**
**AGOSTI 2021**
**MUDA: 2 ½**

# MTIHANI WA GOLDEN ELITE

# JUZUU YA KWANZA

**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**INSHA**
**Muda: 2 ½**

**MAAGIZO**

- Jibu maswali yote.

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

*Karatasi hii ina kurasa 9 zilizopigwa chapa*

***Geuza ukurasa***

**1. UFAHAMU**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali*.**

Ingawa wenye hekima walisema kuwa macho hayana pazia, ni muhimu kuyatumia macho ulivyojaliwa na muumba wako. Ndio maana ninaamini pia kuwa macho hayafilisi duka! Mimi hupenda kuyafumbua macho pima kila nitembeapo barabarani au hataninapokaa nyumbani kusakura yaliyo karibu nami. Lakini, kuna matukio ambayo hunisumbua na kunisikitisha. Hunisumbua kwa sababu sipati majibu kwao; hunisikitisha kwa sababu ya athari zake na mihemko yanayoleta katika hisia zangu za ndani. Kila mara hujiuliza: "Kwa nini watu wengi huteseka namna hii duniani? Kwa nini mtu adamke mafungulia ng'ombe akielekea kibaruani kila siku bila kusita huku wachache wakistarehe? Kwa nini ugonjwa unaweza kumvamia mtu ghafla bin vuu na kumlemaza ama kumtaabisha kwa muda mrefu kabla ya kumwuua? Kwa nini? Mbona kila mara mtu anapokuwa akisikitika kuna mwenzake huwa anacheka? Ama maisha ni kitendawili tu?"

Hata hivyo, linalonishangaza sana wakati mwingine ni jinsi wale wanaowafikiria kuwa wanataabika wanavyochukulia hali zao. Utawaona akina yakhe wakitabasamu kila mara na kucheka hata matumbo yakiwaguruma. Utawasikia wakiulizana: 'Umeshindaje?' Kana kwamba wameshindia karibu kwa kila hali. Mbona wasiulizane: 'Umeshindwaje?'

Hii ndio sababu wakati mwingi moyo wangu huanza kuhisi kuwa labda siku ya kiyama inakaribia zaidi. Wewe hebu fikiria, wanasayansi wanapotuambia kila mara wamevumbua hiki na kile ambacho kitafanya maisha ya mwanadamu kuwa sahihi zaidi, ndivyo tunavyojitumbukiza katika majanga na matatizo zaidi maishani. Hii ndio sababu hata ile dhana iliyoweka miaka ya nyuma kuwa maradhi ya ukimwi ambayo yamekosa tiba hadi sasa kando na kuwaua mamilioni ya watu yalitokana na ajali ya kisayansi huko Marekani inaweza kupata mashiko. Swali la kujiuliza ni: 'Ni kwa nini maisha yanaposemekana kuwa yamebadilika na kuwa mazuri siku hizi ikilinganishwa na zamani mimi naona kinyume? Au wewe waonaje? Mbona zamani, kabla ya majilio ya kila siku hizi kinaitwa 'Maendeleo' watu walikuwa wakitembea tu na kula matunda na mimea, watoto wakicheka na kucheza kwa furaha bila bughudha yoyote? Au hata mbona watu hawakuwa na ubinafsi niuonao siku hizi? 'Maendeleo hayo tunayoyataja kila siku unayaona kama ongezeko la chuki, uhasama, magonjwa, ubinafsi, vita, ufisadi na hujuma dhidi ya mazingira ambamo mwanadamu anafaa kufurahia maisha. Ukweli ni kwamba maendeleo haya yamepelekea watu wengi zaidi ulimwenguni kuishi katika mitaa ya mabanda, kuwa na nyuso za "sitaki mchezo" na "karibu lakini usidowee."

Ninapotazama zaidi katika bahari ya Luja kuhusu ukweli halisi maajuzi nimeishitakia hali hii kwa Mola ingawa sijajaliwa jibu. Hata hivyo, ninavyoendelea kulingoja jibu ndiyo ninavyoendelea kuelewa hii dhana kuwa ulimwengu ni kokwa ya fuu huishi utamu, anayekwisha ni binadamu.

(a) Kwa nini mwandishi anadai kuwa labda siku ya kiyama imefika? ( alama 2 )

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

(b) Unafikiri ni kwa nini mwandishi anayaona madai kuhusu maendeleo duniani kuwa ni ya kinaya? ( alama 2 )

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

(c ) Mwandishi wa taarifa anamaanisha nini kwa kusema "sitaki mchezo" na "karibu lakini usidowee" ( alama 2 )

(d) Yalinganishe maisha ya "Kabla ya maendeleo" na ya sasa ambayo mwandishi anadai ni duni kuliko ya zamani. ( alama 2 )

(e) Je, unakubaliana na msimamo wa mwandishi kuwa madai kuhusu maendeleo ni kinaya? Eleza. ( alama 2 )

(f) Eleza maana ya vifungu hivi vya maneno kama vilivyotumika katika taarifa. ( alama 3 )

(i) Kusakura

(ii) Macho hayafilisi duka

(iii) Bahari ya luja.

**2. MUHTASARI ( alama 15 )**

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Miaka mingi ya kutawaliwa na wakoloni iliwafanya wananchi wengi kupuuza umaarufu na uadilifu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa kwa manufaa ya kuarifiana habari mbalimbali kwa ufasaha na kuelewana vyema. Wakoloni pia waliwashawishi wananchi waone kana kwamba lugha ya Kiswahili ni kwa ajili ya watu wale wasiokuwa na elimu na wale ambao hawajastaarabika kwa wale wenye elimu na wastaarabu. Wakoloni waliwashawishi kuamini kwamba lugha ya kigeni yaani Kiingereza ndiyo hasa lugha inayofaa kwa kujieleza na kufahamishana habari.

Kutokana na vikwazo hivi, si ajabu kuona hadi sasa mwananchi halisi akijitwaza kwamba hawezi kujieleza kwa ufasaha au kumpasha mwenzie habari kwa ukamilifu mpaka atumie lugha ya Kiingereza.

Hata katika ofisi nyingine za serikali hadi hii leo, japo imeisha kupitishwa kisheria kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya taifa, bado utawaona wananchi wengine wanapendelea kuzungumza Kiingereza wao kwa wao, ili wajulikane kwamba wana kisomo na wamestaarabika. Vikwazo vya namna hii vimewalemea wananchi hasa kwa upande wa magazeti. Utaona mwananchi ambaye anafahamu Kiingereza kidogo sana, akijinunulia gazeti kubwa la kiingereza na kuanza kuzurura nalo kutwa nzima bila kwambulia mengi ndani yake. Pia utawasikia wananchi wengi wakidai kwamba hawataki kusoma magazeti ya Kiswahili kwa sababu inakuwa vigumu kwao kuelewa mambo yaliyomo kama vile ambavyo wangalielewa katika gazeti la kiingereza. Mabeberu wameshagundua kwamba tunao upotofu wa aina hiyo, ndipo unaona mara nyingi wanawaletea wananchi magazeti mengi ya kiingereza, mengine yakiwa na nia ya kuwapotosha wakijua kwamba watayasoma tu mradi yameandikwa kwa lugha ya kiingereza.

Mara nyingi taifa fulani la kibeberu likitaka tuchukiane na taifa jingine fulani ambalo ni adui yake kisiasa au kiuchumi, taifa hilo la kibeberu linaandika habari za uchochezi kwenye magazeti yao ya lugha ya kiingereza mambo kuhusu taifa lile adui yake. Magazeti hayo huandikwa kwa lugha nadhifu ya kiingereza na kuletewa wananchi hapa nchini. Maskini wananchi wengine waliopotea kwa kudhani kiingereza ndiyo lugha nzuri ya kigazeti, wanayanunua mara moja na kuanza kuyasoma magazeti hayo na pia kuwapa watoto wao wayasome. Matokeo yake ni kwamba bila kujitambua, wanajikuta wanayafanya yale mabeberu waliyotarajia wayafanye, yaani wanaanza kuchukiana bure. Madhumuni ya kuandika habari kwenye gazeti ni kutaka kuwafahamisha wasomaji mambo yaliyotokea au yanayotokea siku hata siku kwa lugha inayofahamika na kueleweka kwa urahisi bila kumtatiza msomaji. Ikiwa basi hiyo ndiyo madhumuni, kuna haja gani kutumia lugha ya kigeni ili kuwaeleza wasomaji wako jambo ambalo wangaliweza kuelezwa kwa lugha yao jambo ambalo wanaifahamu vyema? Mtu aelezapo jambo kwa maandishi akitumia lugha yake mwenyewe ambayo anaifahamu vyema undani wake, huelezea jambo lenyewe kutoka moyoni na akilini kwa njia adili ambayo yeye mwenyewe anaielewa vyema na pia wasomaji wake wataielewa kwa ukamilifu. Kwa jumla, jambo ambalo mwandishi ataliandika kwa lugha ambayo ni ya asili yake na ambayo anaielewa vyema halitamtatiza msomaji wake ambaye pia anaielewa vyema lugha hiyo.

***Maswali***

(a) Ni athari gani ambazo zinadhihirisha kuwa wananchi huipuuza lugha ya Kiswahili.
( Maneno 50-60) ( alama 9, 2 mtiririko )

Matayarisho

Jibu

(b) Eleza ujumbe uliomo katika aya ya mwisho. ( Maneno 45 -55 )

( alama 6, 1 mtiririko)

Matayarisho

Jibu

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Linganisha na tofautisha sauti / p/ na /m/. ( alama 2 )

(b) Toa mfano wa neno lenye muundo wa silabi ya sauti mwambatano na ubainishe. ( alama 2 )

(c ) Ainisha kifungutenzi kifuatacho. ( alama 3 )
Kilichopigiwa

(d) Tunga sentensi moja yenye muundo ufuatao wa maneno. ( alama 2 )
W + V + T + E

(e) Tunga sentensi ukitumia nomino <u>changarawe</u> ili kudhihirisha upatanisho wa kisarufi ( alama 2)

(f) Yakinisha
Usipoziba ufa utajenga ukuta. ( alama 2 )

(g) Unda nomino mbili tofauti kutokana na kitenzi kosa. ( alama 2 )

(h) Andika upya sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendwa.
Hakimu amemhukumu mshatakiwa. ( alama 2 )

(i) Tunga sentensi ukitumia neno <u>popepole</u> kama : ( alama 2 )
(i) Kielezi

Nomino ______________________________

(j) Tambua na ueleze aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo. ( alama 3 )
Mama aliwapikia watoto chakula kwa sufuria.

(k) Bainisha chagizo katika sentensi ifuatayo. ( alama 1 )
Magaidi huandaa mikutano yao kisirisiri wasijulikane.

(l) Tambua matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari katika sentensi hizi.
(i) Mwalimu alikuwa a<u>k</u>ifunza nilipoigia darasani. ( alama 1 )

(ii) Ana<u>ji</u>dunisha kwa tabia ya kuombaomba. ( alama 1 )

(m) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia michoro ya matawi. ( alama 4 )
Rashid na Rehema walitunga mashairi mazuri sana.

(n) Akifisha sentensi hii ili kuleta maana mbili tofauti. ( alama 2 )
Jirani yangu ameaga dunia.

(o) Andika sentensi ifuatayo katika msemo wa taarifa.
"Huku ndiko mtakakopata maziwa yenu," mwenye duka akasema. (alama 3 )

(p) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa wingi. ( alama 2 )
Mtu huyo alibomoa nyumba kubwa.

(q ) Tambua vishazi katika sentensi ifuatayo.
Nilimwona mamba nilipopiga mbizi majini. ( alama 2 )

(r ) Andika upya kwa kutumia o-rejeshi tamati.
Kitabu ambacho tunasoma kitatufaidi. ( alama 2 )

**SWALI LA 4: ISIMU JAMII**

Eleza changamoto zinazokumba ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. ( alama 10)

Jina ____________________________________________ Nambari ______________________________

Sahihi ya mtahiniwa ___________________

Tarehe _______________________________

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**AGOSTI 2021**
**MUDA: 2 ½**

# MTIHANI WA GOLDEN ELITE

# JUZUU YA KWANZA

**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**Muda : 2 ½**

**MAAGIZO**

- Jibu maswali **MANNE** pekee.
- Swali la **KWANZA** ni la **LAZIMA**.
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakia.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

***Karatasi hii ina kurasa 3 zilizopigwa chapa***

***Geuza ukurasa***

**<u>Swali la lazima</u>**

**1. <u>SEHEMU YA A: Ushairi</u> (ALAMA 20)**

***<u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali</u>***

Wanafunzi sikieni, niwape wangu wasia
Mkiwa mtihanini, muweze kuzingatia
Nataka mtambueni, Msije mkajutia
Kwa bidii darasani, mtihani mfaulu

Kufanikiwa kitaka, watii nao walimu
Sielekeze **dhihaka**, kwao wao ni muhimu
Kwauliza mwahitajika. maswali yalo magumu
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

M rauke na mapema, msome kwa tumaini
Msije nyie kukwama. kwenye wenu mtihani
Muweze rudia vyema, mlofunzwa awalini
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Umoja ni nguvuni, Mwafaa mfahamuni
Jiunge na makundini, masoma mujadilini
Na lile lilo gizani, takuja kulionani
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Ilopita mitihani, kwa chudi irudieni
Mpate na taswirani, ya ule ulo mwishoni
Ya ziada kazini, ifanye sizembeeni
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mwelewe sana vyema, yaliyo mtaalani
Msije mkandama, Cha mtihani chumabni
Mgongeni ndipo vyema, sije mkapoteani
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mkiwa madarasani, kelele muepukeni
Sije mkapotezani, muda wenu masomoni
Neneni na vitabuni, vitakuja walipani
Kwa bidii durusuni. mtihani mfaulu

Michezo sipuuzeni, kwayo nyie burudika
Nishati ntapatani, kifurahia michezo
Mazoezi eleweni, ni muhimu kwa ubongo
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Nimefika kaditama, kuweleza ya moyoni
Yafwateni hayo mema, mfaulu mtihani
Ni upuzi msiseme, muda wangu potezeni
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

**Maswali**

(a) Eleza mawaidha yanayotolewa kwa wanafunzi kuhusu namna ya kujitayarisha Vyema kwa mtihani (alama 5)

(b) Eleza umbo la shairi hili (alama 4

(c) Eleza mbinu tatu zilizotumiwa katika shairi hili ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi (alama 3)

(d) Taja na utoe mfano wa tamathali moja ya usemi iliyotumiwa katika shairi hili (alama 1)

(e) Eleza toni ya shairi hili (alama 1)

(f) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya mjazo (alama 4)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi

i) Dhihaka

ii) Kaditama

**SEHEMU YA B: RIWAYA**

**CHOZI LA HERI (Assumpta K matei)**

**(Jibu swali la 2 au 3)**

**2. *"Sandarusi zenyewe mtu anazitafuta kwenye milima ya taka zinazotolewa huko waishio waheshimiwa kuja kutupwa huku."***

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

b) Kwa kurejelea mifano mingine **minane**, fafanua maudhui yanayoangaziwa na maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 16) .

**4.** Kwa kutumia hoja kumikumi eleza jinsi maudhui ya utu na uozo na kijamii yalivyoshughulikiwa katika chozi la Heri (alama 20)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**

**KIGOGO (Pauline Kea)**

***(Jibu swali la 4 au 5)***

**4.** ‘’ Nimekuja kuwakomboa”

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili ( alama 4)

**b)** Kwa kutumia hoja kumi na mbili, thibitisha kuwa msemewa na wenzake walistahili Kukombolewa(alama 12)

**c)** Kwa kutumia hoja nne eleza umuhimu wa msemewa ( alama 4)

**5**. Tamthilia ya kigogo ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika. Thibitisha (alama 20)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

**TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

*(Jibu swali la 6 au 7)*

**6.**” Licha ya…..ninayopewa na wazazi wangu naona bado kuna pengo kubwa maishani mwangu

**a)** Weka dondoo katika muktadha wake (alama 4)

**b)** Fafanua pengo linalorejelewa na msemaji ( alama 2)

**c)** (Thibitisha kuwa hatua za kujaza ‘pengo’ ulilolifafanua hapo juu ulikumbwa na vizingiti vya kitabaka ( alama 8)

**d)** (Onyesha hulka sita za msemaji wa dondoo hili (alama 6)

**7.** Onyesha jinsi wahusika wafuatao wanavyochangia katika kufanikisha maudhui kwenye hadithi ya masharti ya kisasa:

(a) Kidawa

(b) Dadi

**SEHEMU YA E:**

**FASIHI SIMULIZI**

8. ***Mwanangu dunia haitaki papara. Ikiwa unataka kufanikiwa katika mustakabali wako kuwa mtoto mtiifu na mwongofu. Kumbuka kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu….’’***

(a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 1)

(b) Eleza sifa tano za kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 5)

(c) Fafanua dhima nne za kipera hiki katika jamii (alama 4)

(d) Fanani anawezaje kuihusisha hadhira katika usimulizi wake? (alama 4)

(e) Eleza majukumu sita ya nyimbo katika uwasilishaji wa ngano (alama 6)